JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

UJUMBE WA WAZIRI WA UCHUKUZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB), KUELEKEA MKUTANO WA SABA WA DUNIA WA USAFIRI WA ANGA WA SHIRIKA LA KIMATAIFA LA USAFIRI WA ANGA (ICAO), TAREHE 16–20 NOVEMBA 2026, MONTRÉAL, CANADA



MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB)
WAZIRI WA UCHUKUZI

Salamu!

Imepita zaidi ya miaka kumi na mitatu tangu jumuiya ya kimataifa ya usafiri wa anga ilipokutana katika Mkutano wa Sita wa Dunia wa Usafiri wa Anga wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO ATConf/6), uliofanyika jijini Montréal mwezi Machi 2013. Tangu wakati huo, sekta ya usafiri wa anga duniani imepitia mabadiliko makubwa, yaliyoleta fursa mpya na wakati huo huo kuibua changamoto zinazohitaji ushirikiano mpya wa kimataifa, ubunifu na dhamira ya pamoja.

Usafiri wa anga duniani umekua kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha mwaka 2012 hadi 2026. Kwa mujibu wa Makadirio ya Muda Mrefu ya ICAO (ICAO Long-Term Forecast) na Ripoti ya Mwaka ya ICAO ya 2024, idadi ya abiria waliosafirishwa kwa safari za ratiba ilikuwa bilioni 3.0 mnamo mwaka 2012, na inakadiriwa kufikia bilioni 5.1 mnamo mwaka 2026, sawa na ongezeko la asilimia 70. Kwa upande wa miruko ya ndege, sekta inakadiriwa kukua kwa zaidi ya asilimia 21 kutoka miruko milioni 31.6 iliyorekodiwa mwaka 2012.

Usafiri wa anga unaendelea kuwa na nafasi muhimu katika kuunganisha uchumi wa mataifa, kuwezesha biashara ya kimataifa, kukuza utalii na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Wakati huo huo, ongezeko la mahitaji ya abiria, maendeleo ya teknolojia, mabadiliko ya mwenendo wa soko, pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya ugharamiaji wa miundombinu, vinaendelea kubadili mustakabali wa usafiri wa anga wa kimataifa.

Mkutano wa Saba wa Dunia wa Usafiri wa Anga wa ICAO (ATConf/7), unaotarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 16 hadi 20 Novemba 2026 chini ya kaulimbiu isemayo “Usafiri wa Anga: Kichocheo cha Kuunganisha Dunia, Maendeleo ya Kiuchumi na Ustahimilivu katika Ulimwengu Unaobadilika,” utakuwa jukwaa muhimu kwa Nchi Wanachama na wadau wa sekta kujadili vipaumbele muhimu vya kisera, fursa za uwekezaji na ubia wa kimkakati unaolenga kuendeleza usafiri wa anga kwa njia endelevu, kuimarisha muunganiko wa dunia, na kuongeza ustahimilivu wa sekta ya usafiri wa anga.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua usafiri wa anga kama nyenzo ya kimkakati ya kuwezesha maendeleo ya Taifa, mtangamano wa kikanda, biashara ya kimataifa, utalii na uwekezaji. Kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Serikali imedhamiria kujenga mfumo wa uchukuzi wa kisasa, shindani, endelevu na jumuishi wenye uwezo wa kuwezesha mageuzi ya kiuchumi na kijamii ya muda mrefu.

Kwa kutambua fursa hizi, Serikali inaendelea kutoa kipaumbele katika kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege, kuimarisha uwezo wa shirika la ndege la Tanzania, kuboresha huduma za uongozaji ndege, kuimarisha usimamizi wa usalamawa usafiri wa anga, pamoja na kufungua sekta ya usafiri wa anga kimataifa.

Uwekezaji wetu katika miundombinu ya usafiri wa anga, ikiwemo ujenzi wa viwanja vipya vya ndege na uboreshaji wa vilivyopo unaoendelea, unalenga kuimarisha nafasi ya Tanzania kama lango la kimkakati la usafiri wa anga, kuimarisha muunganiko kati ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini, na kuunganisha ukanda huu kwa ufanisi zaidi na masoko ya kimataifa.

Vilevile, Serikali inatambua kuwa uendelezaji wa miundombinu pekee hautoshi kufungua uwezo kamili wa kiuchumi wa sekta ya usafiri wa anga. Ukuaji endelevu unahitaji mazingira wezeshi ya kisera na ya usimamizi, mbinu bunifu za ugharamiaji, ubia madhubuti kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, uwezo imara wa kitaasisi, na uwekezaji endelevu katika kuendeleza rasilimali watu.

Katika muktadha huo, Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za kikanda na kimataifa zinazolenga kuimarisha muunganiko wa usafiri wa anga, ikiwemo utekelezaji wa Soko Moja la Usafiri wa Anga Afrika (SAATM), ambalo linatoa fursa muhimu za kupanua masoko, kuimarisha mtangamano wa kikanda, na kuwezesha biashara na utalii barani Afrika.

Wakati jumuiya ya kimataifa ya usafiri wa anga ikitafakari mbinu mpya za udhibiti wa kiuchumi, upatikanaji wa masoko, ugharamiaji wa miundombinu, ubunifu na ustahimilivu wa sekta, Tanzania inasisitiza umuhimu wa kuhakikisha kuwa manufaa ya ukuaji wa usafiri wa anga yanagawanywa kwa usawa miongoni mwa Nchi zote, hususan nchi zinazoendelea. Tanzania inaamini kwa dhati kuwa mustakabali wa usafiri wa anga wa kimataifa unapaswa kujengwa juu ya ushirikiano imara wa kimataifa, fursa jumuishi za kiuchumi, ubunifu wa kiteknolojia, uwajibikaji katika utunzaji wa mazingira, na dhamira isiyoyumba ya kuzingatia viwango vya juu kabisa vya usalama wa usafiri wa anga.

Tunapoelekea mwaka 2050, azma yetu ya pamoja inapaswa kuvuka lengo la kuhimili ongezeko linalotarajiwa la safari za usafiri wa anga, na kuhakikisha kuwa ukuaji huo unakuwa kichocheo cha maendeleo endelevu ya kiuchumi, ustawi wa pamoja, na fursa zenye tija kwa mataifa yote.

Kwa msingi huo, Mkutano wa Saba wa Dunia wa Usafiri wa Anga ni fursa adhimu ya kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kuweka mwelekeo wa kisera utakaoongoza mustakabali wa usafiri wa anga duniani. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inathibitisha tena dhamira yake ya kushirikiana kwa karibu na ICAO, Nchi Wanachama, mashirika ya kikanda, washirika wa maendeleo na wadau wa sekta ili kujenga mfumo wa usafiri wa anga duniani wenye muunganiko zaidi, ufanisi, ustahimilivu, uendelevu na unaofikiwa na wote.